

Barikiwa, Mwokozi mwema

traduit de « Béni sois-tu, Sauveur fidèle »

♩ = 80
Polepole kadiri na tukionyesha
mf

219

1. Ba - ri - ki - wa, Mwo - ko - zi mwe - ma
2. We - we mu - be - ba - ji wa mbe - gu
3. Mbe - gu ya nga - no u - do - ngo - ni,
4. Ma - vu - no sa - sa ni ta - ya - ri
5. U - ta - o - ne - ka - na kwa si - fa

U - li - ye tu - te - mbe - le - a
U - li - zi - pa - nda kwa cho - zi,
I - ki - fa, i - a - ndi - kwa - vyo,
Mbe - le ya - ko, mu - pa - nda - ji ;
Si - si Tu - ki - ku - zu - ngu - ka,

p
U - ki - fu - ni - ka u - tu - ku - fu
U - ka - pa - ta ma - te - so, Ye - su
Ha - i - ta - ba - ki pe - kee ya - ke
U - ta - ru - di, u - kii - mba ra - ha,
Si - si ma - tu - nda ya u - shi - ndi,

mf

Ha - ta ku - fa - na - na mu - tu.
 Ka - ti - ka ku - ji - to - le - a.
 I - la i - ta - zaa ma - tu - nda.
 U - ki - ya - shi - ka ma - su - ke.
 Tu - ki - ku - sa - nywa mi - le - le.